

Athari ya Ukiushi wa Kisarufi katika Tafsiri ya Matini katika Majukwaa ya Kidijiti

Mark A. Odawo¹, Carren Nyandiba¹ na James Omari Ontieri²

¹Chuo Kikuu cha Rongo

¹Chuo Kikuu cha Rongo

²Chuo Kikuu cha Maasai Mara

Ikisiri

Jukumu la kimsingi la lugha kama mfumo wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi ni kukidhi mahitaji ya mawasiliano mionganii mwa watumiaji wake. Lugha hupata uamilifu huu pale vipashio vyake vinapopangwa kulingana na kanuni za kimofosintaksia za lugha hiyo. Mpangilio huu ndio unaozalisha matini zenye mshikamano na ambazo hujitosheleza kimaana. Hata hivyo, dhima hii inaweza kuvurugwa pale ambapo maana inayowasilishwa katika lugha fulani imefumwa kutokana na tafsiri. Japo matini chanzi inatarajiwa kuchakatwa kwa usadifu katika matini lengwa, kadhia ya tafsiri na tofauti kati ya lugha chanzi na lugha lengwa huweza kufisidi maana. Hali hii huelekea kudhihirika zaidi kutokana na maendeleo ya Tehama ambayo yameathiri pakubwa matumizi ya lugha ikiwemo taaluma ya tafsiri. Ni kutokana na hoja hii ambapo makala haya yanaangazia jinsi ukiushi wa kisarufi unavyoathiri maana ya matini tafsiri katika Majukwaa ya Kidijiti. Uteuzi wa kimakusudi ulitumiwa ili kupata sampuli sadifu ya data kutoka tuko.com na bbc.com. Data zilizokusanya na zilichanganuliwa kinathari huku majedwali yaktumiwa kuweka wazi matokeo. Matokeo ya utafiti huu yanatazamiwa kuwa na umuhimu wa kutoa maarifa kuhusu mbinu na mikakati ya uhawilishaji waujumbe wenye muumano kwa watafsiri wa matini asilia na za mtandaoni. Waaidha, kazi hii itanufaishamashirika ya uanahabari na wanahabari huria wanaonua kuboresha tafsiri za taarifa zao na vilevile kuchochea wasomi wanaonua kutafiti kuhusu masuala ya kipragmatiki yanayodhihirika katika tafsiri za lugha mbalimbali.

Maneno Muhimu: Athari, Ukiushi, Tafsiri, Sarufi

Utangulizi

Lugha hudumisha uamilifu wake wa kutumika katika kujieleza na kupidisha maarifa inapotumiwa kwa kuzingatia kanuni zake. Maarifa anayohitaji binadamu nayo hupatikana na kupidishwa kwa lugha mbalimbali. Kauli kuwa jamii za binadamu ulimwenguni ni za asili na tamaduni tofauti humaanisha kuwa haziwezi kuelewana kikamilifu na kupasha ujumbe zinapotumia lugha zao za asili. Hali hii hupelekeea haja ya kubadilisha maana ya matini kutoka lugha moja hadi lugha nyingine ya wapokezi wa ujumbe kupitia taaluma ya tafsiri.

Watalamu mbalimbali kama vile (Catford, 1965; Nida na Taber, 1969; Larson, 1984; Newmark, 1988; Mwansoko, 1996; Wanjala, 2011) wanaafikiana kuwa tafsiri ni mchakato wa mawasiliano unaohusu uhamishaji wa maana na ujumbe ulio katika lugha chanzi (kuanzia hapa LC) hadi lugha lengwa (kuanzia hapa LL). Lengo kuu la tafsiri ni kuwasilisha maana iliyomo kwenye matini chanzi (kuanzia hapa MC) kwa kutumia matini lengwa (kuanzia hapa ML) ili kuathiri hadhira lengwa (kuanzia hapa HL) kwa namna inayofanana na ile waipatayo hadhira chanzi (kuanzia hapa HC). Kwa mantiki hii, tafsiri hujitokeza sawa na uhusiano unaoipa ML hadhi ya kuchukuliwa kama toleo jipya la MC. Kama anavyosema Mwansoko (2016), tafsiri kwa dhati yake ni daraja linalouganisha jamii mbalimbali zenye lugha zinazotofautiana na kwamba bila tafsiri, isingewezekana kwa jamii hizo zinazotumia lugha tofauti kupata maarifa, ujuzi na utamaduni wa jamii nyingine.

Kuchipuka kwa maarifa na ujuzi katika taaluma mbalimbali za kisayansi, kiufundi, kisheria, kibashara na katika nyanja nyinginezo za kimaendeleo katika ngazi ya kimataifa, kumezidisha haja ya kutafsiri matini anuwai ili kuwezesha usambazaji wa haraka wa maarifa katika kufanikisha mawasiliano timilifu. Oduori (2008) anasema kuwa taaluma zinavyopanuka, uvumbuzi huendelea kuwepo. Maarifa yanayotokana na uvumbuzi huo huhitaji kusambazwa ili kuwafikia watu katika upande mwengine wa ulimwengu kwa lugha wanayoilewa vizuri. Hivi ni kusema kuwa tafsiri inategemewa sana katika kufanikisha mawasiliano na kusambaza maarifa katika dunia ya leo inayoendelea kuwa kijiji kidogo.

Maendeleo katika Tehama yamechangia mabadiliko makubwa katika uwasilishaji wa habari. Hii ina maana kuwa pana mwelekeo wa kuhama kutoka utegemezi wa nyenzo zilizozoleka za kusambaza taarifa kama vile redio, televisheni, magazeti na majarida. Kama anavyosema Shitemi (2007), mawasiliano ya kitehama hasa katika sanaa za burudani, maonyesho ya filamu na uhabarishaji katika vyombo vy'a habari yamepanua dhima ya tafsiri za kielektroniki. Leo, utandawazishaji wa taarifa umewezeshwa kwa wepesi wa ajabu kupitia Majukwaa ya Kidijiti (kuanzia hapa MK). Japo uwasilishaji wa taarifa zilizotafsiriwa mtandaoni kwa Kiswahili ni tukio la miaka ya hivi majuzi,

watu wanaofutilia na kutegemea MK ili kupata habari huzidi kuongezeka kila uchao.

Watu wengi wanachangamkia majukwaa haya kutokana na uwezekano wa kupata taarifa nyingi mahali popote punde tu zinapochipuka. Taarifa ambazo kimsingi huandikwa kwa LC ya Kiingereza pia huifikia umma kutokana na tafsiri katika LL ya Kiswahili kupitia MK. Hata hivyo, changamoto za kutafsiri taarifa zinazozalishwa katika MK zimekuwa kikwazo dhidi ya dhima ya kimsingi ya lugha ya kufanikisha mawasiliiano na kusambaza maarifa. Ni kwa misingi hii ambapo makala haya yanajadili jinsi ukiushi wa kisarufi unavyotatiza tafsiri matini katika MK.

Makala haya yanahuus usomaji wa matini ili kudondoa data yakini kutoka MK kupitia rununu na tarakilishi. Matini zilizotambuliwa na kudondolewa ni zile zilizoangazia ufumaji wa maana katika matini za kisiasa, kijamii, kiuchumi na michezo zilizotafsiriwa kutoka LC ya Kiingereza kwenda LL ya Kiswahili kwenye MK.

Katika makala haya, uteuzi wa kimakusudi unatumwiwa ili kupata sampuli sadifu kutoka majukwaa ya *tuko.com* na *bbc.com*. Majukwaa haya huwa na matini nyingi zaidi zilizotafsiriwa moja kwa moja kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kwa ukamilifu na uwazi zaidi. Data zilizokusanywa na kuchanganuliwa kinathari pamoja na majedwali zilijumlisha misamiati, virai, vishazi na sentensi.

Utafiti huu uliegemezwu katika Nadharia ya Ufasiri iliyoasisiwa na Seleskovitch (1968). Kwa mujibu wa Seleskovitch, tafsiri ni zaidi ya mfanyiko wa kiisimu ambapo lugha moja huandikwa kwa kutumia vipashio vya lugha nyingine. Anaona tafsiri kama mchakato wenyewe hatua tatu zinazochangiana na kushikamana: kutambua maana au ujumbe katika MC; kubainisha au kuunda wazo linalotokana na ujumbe huo bila kutawaliwa na miundo ya kiisimu na kuandika upya wazo linalotokana na ujumbe huo katika LL. Kulingana na nadharia hii, mchakato huu wa kihatua ndio unaowezesha matini ya LC kutafutiwa fahiwa na kuhawilishwa katika LL.

Ukiushi wa Kisarufi

Jukumu la kimsingi la lugha kama mfumo wa maana unaowakilishwa kwa maumbo ya kisarufi ni kukidhi mahitaji ya mawasiliiano mionganoni mwa watumiaji wake (Halliday na wenzake, 1964). Lugha hupata uamilifu huu baada ya vipashio vyake kupangwa, kufuatishwa na kuhuishwa na kanuni za kimofosintaksia za lugha hiyo. Mpangilio huu ndio unaozalishwa matini zenye kuzingatia sarufi, ukubalifu na mshikamano na ambazo hujitosheleza kimaana. Hata hivyo, ujumbe unaowasilishwa katika ML wakati mwengine hutatiza kutokana na ukiushi wa kisarufi.

Ukiushi wa kisarufi ni uundaji wa tungo za kisintaksia usiozingatia kanuni za kisarufi za lugha husika. Huku tofauti za maumbo na miundo kati ya LC na LL zikidhihirisha ukiushi huu katika uzalishaji wa ML, unyambuaji mbovu wa mofu na uakifishaji mbaya huweza kuzalisha matini zenye ukakasi hata ndani ya lugha moja. Utafiti wetu umebainisha ukiushi wa kisarufi unaotokana na tofauti za kisintaksia kati ya LC na LL, matatizo ya kiupatanishi, matatizo ya kiuakifishaji, matatizo ya unyambuaji na matatizo ya kitahajia.

Tofauti za Kisintaksia kati ya LC na LL

Kila lugha ina upekee wake wa kupanga na kufuatisha vipashio vyake vya kiisimu kwa mujibu wa kanuni zinazoidhibiti. Kihore (2005) anasema kuwa kila lugha huwa na kanuni na taratibu zake za kupanga maneno kuunda sentensi. Anaeleza zaidi kuwa mipangilio hii inaweza kukaribiana kwa lugha za jamii moja na ikatofautiana sana baina ya lugha za jamii tofauti. Kusema hivi ni kumaanisha kuwa maafikiano ya kumuundo baina ya lugha mbili tofauti hayatokei kwa urahisi. Wills (1983) anafafanua kuwa tofauti ya tafsiri huweza kutokea kwa sababu hakuna lugha iliyo sawa na nyingine kumuundo na kimaana. Tofauti kati ya Kiswahili na Kiingereza zinaweza kupatikana katika udhihirishaji wa kiima, mpangilio wa vivumishi na nafasi ya chagizo.

Kwa kawaida, mpangilio wa vipashio vya kisintaksia katika lugha ya Kiingereza ni ule wa kitenzi, kiima na yambwa. Mpangilio huu haulandani na wa Kiswahili ambapo kiima hutangulia kitenzi na kufuatwa na yambwa. Kwa sababu ya tofauti hizi, mfasiri anaweza kupotosha ujumbe anapokosa kumudu miundo ya ndani ya lugha zinazoshirikishwa katika tafsiri. Mfasiri wakati mwingine hupata ugumu katika jitihada za kutatta changamoto hizi za kiisimu anapohawilisha ujumbe na hujikuta akizingatia aina ya tafsiri ya neno kwa neno ambayo kwa kiasi kikubwa hudumisha muundo wa LC katika LL. Tafsiri kengeushi inayoleta utata wa kimawasiliano hutokea pale ambapo miundo ya kisarufi ya LC inalazimishwa katika LL. Kinachomaanishwa hapa ni kuwa harakati za kuhifadhi vipashio fulani vya LC katika LL zinaweza kusababisha mpangilio wa vipashio vya kiisimu katika ML kwa njia inayoathiri maana. Tazama tafsiri ifuatayo ya matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Matini Chanzi:

Ezra Chiloba loses case challenging *his* suspension by IEBC chairman Wafula Chebukati...**The Chairman's decision** made him culpable for contempt. A **determined Chiloba** filed another application seeking his reinstatement and was awarded temporary orders to resume office but met with another suspension letter a few hours after the ruling which was delivered on Thursday, June 14.

Matini Lengwa:

Ezra Chiloba apoteza kesi ya kупinga kusimamishwa kazi *kwake* na mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati...*Uamuzi wa mwenyekiti* ulimfanya kupatikana na hatia ya kudharau korti...*Chiloba mwenye ari* aliwasilisha kesi nyingine kwa madhumuni ya kurejeshwa kazini na akapatiwa amri ya muda ya kurejea afisini lakini akakumbana na barua nyingine ya kumsimamisha kazi saa chache baada ya uamuzi uliotolewa mnamo Alhamisi, Juni14.

Harakati za kuhifadhi vipashio fulani vya LC katika LL huweza kusababisha mpangilio wa vipashio vya kiisimu katika ML kwa njia inayoathiri maana. Sentensi ‘Ezra Chiloba apoteza kesi ya kупinga kusimamishwa kazi na mwenyekiti wa IEBC Wafula Chebukati’ ingeleweka zaidi bila matumizi ya kivumishi ‘kwake’. Utokeaji wa kivumishi hiki katika sentensi hii unatatiza maana kwa kuwa matumizi yake yanabainika kama urudiaji usiohitajika wa kiima ‘Ezra Chiloba’ ambaye amekwishatajwa mwanzoni mwa sentensi. Upenyezaji wa kivumishi hiki unajitokeza kama harakati za kutafsiri kimilikishi ‘his’ ambacho kimejitokeza katika MC.

Kwa upande mwingine, tafsiri ya ‘*The Chairman’s decision...*’ kama ‘*Uamuzi wa mwenyekiti...*’ imesababisha uchopekaji wa kitendi ‘ulimfanya’ katika ML. Kwa sababu hii, ML ‘Uamuzi wa mwenyekiti ulimfanya kupatikana na hatia ya kudharau korti’ inaleta utata wa kisemantiki. Mpangilio wa ‘Mwenyekiti alipatikana na hatia ya kudharau korti kutokanana uamuzi wake’ ungefaa zaidi katika kuibua maana iliyokusudiwa kwa njia ya moja kwa moja. Katika sehemu hii, maana ingeleweka kwa uwazi zaidi kwa kupenyeza kihuishi ‘kutokana na’ badala ya kitendi kisaidizi ‘ulimfanya.’

Kulingana na nadharia ya Ufasiri, mfasiri anatarajiwa kufahamu na kutumia LL vilivyo. Hii ina maana kuwa mfasiri anapaswa kutambua na kutumia kanuni za kiisimu na matumizi ya kileksia ya lugha inayotumiwa katika ML. Ujuzi wa mtafsiri kuhusu kanuni za kisintaksia na mpangilio wa viambajengo katika vishazi vya LL unaonekana kuwa si mpevu.

Vilevile katika matini hii, kirai, ‘*A determined Chiloba...*’ kimetafsiriwa kama ‘*Chiloba mwenye ari.*’ Kirai hiki kina mushkeli kisintaksia. Ujumbe unaopitishwa hapa unahu Chiloba kukazana kurudi tena kortini akiamini kuwa angerejeshwa kazini kwa kushikilia kuwa hakuhusika na ujisadi. ‘*A determined Chiloba...*’ inatoa dhana yahaja ya kuthibitisha kuwa hana hatia yoyote na kwamba madai ya kuhusika kwake katika ujisadi ni ya uongo. Kwa upande mwingine, kirai ‘*Chiloba mwenye ari...*’ kinatoa dhana ya nguvu au jazba fulani inayomsisimua mtu kufanya jambo. Hakika, dhana hii ya jazba haidhahiriki. Maana inapotoka kutokana na kudumisha muundo wa LC katika LL. Ili kuitisha

ujumbe kwa ufanifu zaidi, kirai hiki kingetafsiriwa kwa kuundwa upya kama ‘*Kwa kushikilia msimamo wake, Chiloba....’*

Uwezekano wa kuunda upya matini hii ili kubua maana kwa uwazi zaidi inadhihirisha kuwa mfasiri aling’ang’ana kulazimisha muundo wa LC katika LL. Mfano ufuatao wa matini ya siasa kutoka jukwaa la *tuko.com* unabainisha uzalishaji wa sentensi yenye ukakasi kufuatia udumishaji wa muundo wa LC katika LL.

Matini Chanzi:

Does Raila Odinga *still want* to be king, or can he be content being a kingmaker? I can’t think of any other Kenyan who’s worked harder and deserves more to be at State House,” argued the Busia county chief.

Matini Lengwa:

Je, Raila *bado yu wataka* kuwa mfalme ama ameridhika na mahala alipo kwa sasa? Sioni Mkenya mwagine ambaye ametoa jasho kama Raila kupigania demokrasia ya nchi hii, Raila anapaswa kuingia Ikulu bila pingamizi,” Ojaamong aliandika Facebook.

Harakati za kutafsiri matini ‘Does Raila Odinga *still want* to be king, or can he be content being a kingmaker?’ sawa na ‘Je, Raila *bado yu wataka* kuwa mfalme ama ameridhika na mahala alipo kwa sasa?’ ni mng’ang’ano wa kulazimisha muundo wa LC katika LL. Ni wazi kuwa ML inatatiza katika usomaji wake na hivyo kufanya ujumbe usieleweke kufuatia kutafsiri ‘*still want*’ kwa maana ya *bado yu wataka*.’ Kama anavyoshikilia Mwansoko (2016), ukiushi huu wa ruwaza za kisarufi za Kiswahili sanifu huzalisha matini zenye ukakasi masikioni.

Aidha, uzalishaji wa ML unaozingatia udumishaji wa muundo wa LC katika LL husababisha ugeuzaji unaobadilisha nafasi ya vipashio vya kisintaksia katika sentensi. Ugeuzaji huu aghalabu hutatiza udhahiri katika uwasilishaji wa ujumbe. Tazama mfano ufuatao wa matini ya siasa kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Matini Chanzi:

“It’s always a great pleasure meeting with one of Kenya’s most famous sons, President Barack Obama...There is always so much that you can eat. There’s only so bigger house you can have. There’s only so many nice trips you can take...”

Matini Lengwa:

“Kila mara ni furaha kubwa mno kukutana na mtoto wa Kenya ambaye ni maarufu sana, Rais Barack Obama...Kuna mengi ya wewe kula. Kuna jumba kuu zaidi ambalo unaweza kumiliki. Kuna ziara nyingi zaidi za kuvutia unazoweza kwenda...”

Kifungu ‘It’s always a great pleasure meeting with one of Kenya’s most famous sons, President Barack Obama’ cha MCkilichotafsiriwa kama ‘Kila mara ni furaha kubwa mno kukutana na mtotowa Kenya ambaye ni maarufu sana, Rais Barack Obama kimedhihirisha ubadilishaji wa nafasi ya kitenzi na kielezi. Kiswahili kwa kawaida hupanga kielezi baada ya kitenzi. Matini hii inaonesha kinyume ambapo sentensi inaanzia kielezi ‘kila mara...’ kama ilivyo katika muundo wa LC ya Kiingereza ‘It’s always....’ Ujumbe katika taarifa hii bado ungehifadhiwa na hata kueleweka kwa uwazi zaidi kama matini ingeundwa upya kwa kudondosha kielezi hiki katika ML ili kupata matini ‘Ni furaha yangu kukutana na Barrack Obama, rais maarufu mwenye asili ya Kenya.’ Hakika, kielezi hiki hakina uamilifu wa kubainisha umaratokezi wa mikutano kati ya Barrack Obama na Raila Odinga kwa sababu viongozi hawa huwa hawakutani kila mara. Uдумishaji huu wa muundo wa LC katika LL kwa njia inayopelekea upanguaji wa nafasi ya kitenzi na kielezi haukudhihirika tu katika matini za kijamii na kisiasa bali pia katika matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*. Tazama matini ifuatayo:

Matini Chanzi:

“For Real Madrid Cristiano Ronaldo **will always be** one of the great symbols,” said a club statement.

Matini Lengwa:

“Kwa Real, Cristiano Ronaldo **siku zote atakuwa** mchezaji muhimu,” ilisema taarifa ya klubu.

Katika matini hii, MC ‘For Real Madrid Cristiano Ronaldo **will always be** one of the great symbols’ imehamishwa kama ‘Kwa Real, Cristiano Ronaldo **siku zote atakuwa** mchezaji muhimu.’ Tafsiri hii imedhihirisha upanguaji wa nafasi ya kitenzi ‘atakuwa’ na kielezi ‘siku zote.’ Mpangilio wa kufuata muundo wa LL ambao kwao kielezi hufuata kitenzi unapaswa kuwa ‘Kwa Real, Cristiano Ronaldo **atakuwa** mchezaji muhimu **siku zote**.’

M pangilio wa kubadilisha nafasi vipashio vya kisintaksia ili kudumisha mpangilio wa LC umedhihirika pia katika matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*. Katika matini ifuatayo ya kijamii, ugeuzaji uliotokea umebadilisha nafasi ya yambwa na kielezi.

Matini Chanzi:

The prime minister has argued that Canada’s nearly century-old laws criminalizing use of the drug have been ineffective, given that **Canadians are still among the world’s heaviest users.**

Matini Lengwa:

Kiongozi huyo wa chama tawala cha ki Liberaliameeleza kwamba sheria za jadi za nchi hiyo dhidi ya matumizi ya bangi hazifanyi kazi, kuzingatia

kwamba *raia nchini humo ni mionganii mwa wanaotumiwa kwa kiasi kikubwa bangi duniani.*

Katika matini hii, ugeuzaji wa nafasi ya yambwa na kielezi umedhihirika kufuatia kutafsiriwa kwa kifungu ‘Canadians are still among the world’s heaviest users’ kama ‘raia nchini humo ni mionganii mwa wanaotumiwa kwa kiasi kikubwa bangi duniani.’ Katika sentensi hii, yambwa ‘bangi’ imetokea baada ya kielezi ‘kwa kiasi kikubwa.’ Mpangilio ambao ungewasilisha maana kwa uwazi ni ule ambao ungedumisha nafasi ya yambwa na kielezi, yaani ‘raia nchini humo ni mionganii mwa wanaotumiwa bangi kwa kiasi kikubwa duniani.

Inajitokeza kuwa juhudi za kuhifadhi ujumbe wa MC kwa kufuata muundo wa LC zinaweza kusababisha uchopekaji wa vipashio vya ziada vya kisintaksia katika LL. Hali hii wakati mwingine huishia kutatiza maana kama inavyodhihirika katika matini ifuatayo ya kijamii kutoka tuko.com.

Matini Chanzi:

Taking a swipe at corrupt and selfish leaders, Obama said they only showed the ambition to just want to take more and more instead of helping the less fortunate...Obama asked leaders to shun illegal acquisition of wealth and also to ensure there was equity in distribution of resources and knowledge across social and economic divides.

Matini Lengwa:

Akiwakashifu viongozi fisadi na wenye ubinafsi, Obama alisema huwa wanaonyesha ari ya kutaka tu kutwaazaidi na zaidi badala ya kuwasaidia wasiojiweza *jambo ambalo ndilo muhimu*...Obama aliwahimiza viongozi kujitenga na ukusanyaji wa mali kwa njia haramu na kuhakikisha kulikuwa na usawa katika usambazaji wa mali, rasilmali na maarifa katika nyanja zote za kijamii na kiuchumi.

Matini ‘Taking a swipe at corrupt and selfish leaders, Obama said they only showed the ambition to just want to take more and more instead of helping the less fortunate...’ imetafsiriwa kama ‘Akiwakashifu viongozi fisadi na wenye ubinafsi, Obama alisema huwa wanaonyesha ari ya kutaka tu kutwaa zaidi na zaidi badala ya kuwasaidia wasiojiweza *jambo ambalo ndilo muhimu*....’ Jithada za kutunza maana katika matini imepelekea mfasiri kuchopeka kirai ‘...*jambo ambalo ndilo muhimu*.’ Mbali na kuwa si sehemu ya MC, kirai hiki kinaibusha utata katika maana kwa kuwa ujumbe haujitokezi kwa uangavu. Tafsiri wasilifu zaidi ambayo ingehamisha kirai husishi ‘...*badala ya kuwasaidia wasiojiweza*’ kutoka mwisho wa sentensi hadi katikati ingekuwa ‘Akiwakashifu viongozi fisadi na wenye ubinafsi, Obama alisema kuwa *badala ya kuwasaidia wasiojiweza*, huwa wanaonyesha ari ya kutaka tu kutwaa zaidi na zaidi.’ Upanguaji huu ungemwepushia mfasiri changamoto iliyoletwa na vipashio vya ziada vilivyoathiri maana.

Murungi (2012) anasema kuwa katika kuhamisha kazi ya mwandishi asilia, si lazima mfasiri achukue maumbo ya kisarufi ya LC ili kujieleza. Kama inavyosema nadharia ya Ufasiri, analohitaji ni kufahamu yaliyomo katika MC ili kuyawasilisha kwa njia inayokubalika na kufaa kwa HL. Mfasiri anahitajika kufanya hivyo kwa ufundi wa hali ya juu ili asipotoshe maana. Hivi ni kusema kuwa licha ya tofauti kati ya lugha mbili zinazohusika katika kadhia ya tafsiri kuweza kusababisha mabadiliko katika mpangilio wa maneno, virai na vishazi katika sentensi, ufahamu mpevu wa LC na LL unatarajiwa kumwezesha mfasiri kutumia ufundi ili kuchakata tafsiri fanifu.

Nida na Taber (1969) nao wanadai kwamba tafsiri ambayo huzingatia uhamishaji wa maumbo ya LC huathiri ruwaza za kisarufi na kimtindo za LL na hivyo kupotosha maana katika ML. Wanakosoa mwelekeo huu kwa kuongeza kuwa tafsiri ni zoezi la ufasiri wa maana wala sio uhamishaji wa maumbo ya lugha.

Imebainika kuwa kwa kulazimisha miundo ya LC katika LL, maana ya ML hukengeuka. Ili kuepuka hali hii, mfasiri ni sharti kwanza afumbue maana inayowasilishwa katika MC na kisha kuihawilisha kwa uzingativu wa kanuni za kisintaksia za LL. Beecher (1988) anasema kuwa uhawilishaji wa ujumbe kwa utoshelevu kutoka MC humhitaji mfasiri kudumisha miundo ya kisintaksia ya LL. Nadharia ya Ufasiri inamhitaji mfasiri kuwa na uwezo wa kutambua na kutumia kanuni za kiisimu za lugha inayotumiwa katika ML. Ujuzi huu humsaidia mfasiri kufuma upya maana iliyokusudiwa kwa kupanga viambajengo katika kishazi bila kutawaliwa na muundo wa LC. Japo kuna matini nyingi zilizohawilishwa kwa utoshelevu, mwelekeo wa kudumisha muundo wa LC katika uzalishaji wa ML umeibua tafsiri kengeushi.

Matatizo ya Kiupatanishi

Viambishi vipatanishi huambishwa katika vitenzi ili kuleta uwiano wa kisarufi kwa kubainisha ngeli ya nomino husika. Kulingana na Myachina (1981), kitenzi kinapoambishwa kiambishi kiwakilishi cha nomino, ni lazima kiambishi hicho kibainishe ngeli ya nomino iliyotumiwa katika sentensi hiyo. Ikizingatiwa kuwa kwa kawaida sentensi hubeba vipashio vikuu vya kiuamilifu ambavyo ni kiima na yambwa, uambishaji mbaya wa viambishi vya ngeli katika nomino zenye dhima ya kiima na yambwa huweza kukengeusha ujumbe. Matatizo ya kiupatanishi yaliyodhihirika katika utafiti huu ni ya uambishaji mbaya wa viambishi vya ngeli, viambishi virejeshi na viambishi vya vielezi. Tazama uchanganuzi ufuataao:

Mimi ni mwananchi ninayeheshimu sheria na sikuhusika kivyovyyote katika kifo cha Sharon. Nitasaidia kadri niwezavyo katika uchunguzi. **Vitengo vyote vinavyohusika katika uchunguzi huo *uongeze kasi*,**” aliongeza.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*

Soko la kitaifa la uuzaji wa bangi lilifunguliwa saa sita usiku wa kuamkia Jumatano na katika baadhi ya maeneo tayari kulikuwa na misururu ya watu waliosubiri kuhudumiwa huku kukiwepo maswali kuhusu madhara kwa afya, sheria na usalama wa umma. *Hii limezushakazi* kubwa kisheria nchini huku idara zikichagua mifuko isiyobana uuzaji na matumizi ya bangi... Umiliki wa bangi ulikuwa haramu kwa mara ya kwanza Canada mnamo 1923 lakini **matumizi** yake kwa misingi ya dawa *ilihalalishwa* tangu 2001.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*

Katika matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com* iliyonukuliwa hapa, nomino ‘vitengo’ iliyo na dhima ya kiima imepatanishwa vivilivo na kivumishi -ote pamoja na kitenzi kisherikishi ‘husika’ kwa kutumia kiambishi {vi} isipokuwa katika kitenzi ‘ongeza’ ambapo badala ya ‘viongeze’ pametumika ‘uongeze’. Hatua hii inapatanisha nomino ‘vitengo’ katika ngeli ya U-U badala ya ngeli ya KI-VI ili kupata ‘*Vitengo vyote vinavyohusika* katika uchunguzi huo *viongeze kasi*’. Upatanisho mbaya wa kisarufi umedhihirika pia katika matini nyingine ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com* ambapo pana kifungu ‘*Hii limezusha* kazi kubwa kisheria nchini...’ Uambishaji huu umeviruga upatanisho wa kisarufi kwa kuchanganya kiambishi cha ngeli ya I-ZI katika kiashiria ‘*hii*’ na kile cha ngeli ya LI-YA katika kitenzi ‘*limezusha*’ kwenye matini moja. Katika matini hii vilevile, kifungu ‘...lakini *matumizi* yake kwa misingi ya dawai *ilihalalishwa* tangu 2001’, kimepatanisha nomino ‘*matumizi*’ katika ngeli ya I-ZI badala ya YA-YA. Upatanisho unaokubalika unapaswa kuwa ‘...lakini *matumizi* yake kwa misingi ya dawa *yalihalalishwa* tangu 2001.’

Mbali na viambishi vya ngeli, pametokea ukiushi katika upatanishi wa viambishi virejeshi kama inavyodhihirika katika matini ifuatayo:

“Ukweli ni kwamba nimechukua uamuzi huo ili asiwe nahodha wa pili lakinihakuna tatizo lolote kati yetu”, alisema Mourinho. “*Mimi* ndio meneja ninaweza kufanya maamuzi kama hayo”... Kumwachilia Pogba kuondoka kutaonekana kuwa kufeli kwa Mourinho na afisa mkuu mtendaji Ed Woodward, ikiwa ni muda mchache uliopita ambapo mchezaji huyo aliwfurahisha mashabiki katika kombe la dunia. *Ilobaki* ni kusalia naye, lakini hatua hiyo itamaanisha kwamba wadhfa wa Mourinho hauna nguvu tena baada ya kuzuiwa kuwanunua wachezaji wapya aliotaka msimu uliopita.

Chanzo: Matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Matini hii ina upatanishi kiushi katika kifungu ‘*Mimi* ndio meneja ninaweza kufanya maamuzi kama hayo... *Ilobaki* ni kusalia naye...’ Uambishaji huu wa kiambishi kirejeshi {o}unapatanisha kiwakilishi nafsi ‘mimi’ katika ngeli ya U-

ZI badala ya A-WA. Kadhalika, katika ‘*llobaki*’ kumetokea uambishaji wa kiwakilishi {i} badala ya kiwakilishi {li} cha ngeli ya LI-YA umoja. Katika kitenzi hiki pia kumetokea uambishaji wa kiwakilishi kirejeshi {o} badala ya {li} cha ngeli ya LI-YA. Uambishaji unaokubalika unapaswa kuwa ‘*Mimi* ndiye meneja... *Lillobaki* ni kusalia naye...’ Makosa haya ya kiupatanishi yamesababisha uvurugaji wa maana katika matini husika.

Utata wa maana umetokea pia kutokana na kudondoshwa kwa baadhi ya mofu zinazorejelea kiima katika matini. Tazama mifano ifuatayo ya matini ya kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Watu zaidi ya 380 wamethibitishwa kufa baada ya tsunami kusababisha tetemeko la ardhi lenye ukubwa wa richa 7.5 lilopigamji wa Indonesia hapo jana...Tetemeko hili lilianza kwa kutangulia kwa tetemeko lingine dogo *liliua* mtu mmoja na wengine 10 kujeruhwa wakiwa katika soko dogo la samaki huko Donggala.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*.

“Ninafikiria hiki ndicho *kilikosekana* tangu nilipofika Arsenal zaidi ya miaka mitatu iliyopita,” alisema. “Lakini dhidi ya Everton, tuliwashinda chini ya hali ngumu sana. Hivyo, hii ni habari ya kutia moyo sana.”

Chanzo: Matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*.

“Ukweli ni kwamba nimechukua uamuza huo ili asiwe nahodha wa pili lakinihakuna tatizo lolote kati yetu”, alisema Mourinho. “Mimi ndio meneja *ninaweza* kufanya maamuza kama hayo.”

Chanzo: Matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Katika matini ya kijamii ‘...Tetemeko hili lilianza kwa kutangulia kwa tetemeko lingine dogo *liliua* mtu mmoja na wengine 10 kujeruhwa wakiwa katika soko dogo la samaki huko Donggala’, pamedhihirika udondoshaji wa mofu rejeshi {lo} katika kitenzi ‘*liliua*.’ Vilevile katika matini ya michezo ‘Ninafikiria hiki ndicho *kilikosekana* tangu nilipofika Arsenal zaidi ya miaka mitatu iliyopita’, kuna unyofoaji wa mofu rejeshi {cho} katika ‘*kilikosekana*.’ Unyofoaji wa mofu rejeshi {ye}ya kiima umetokea pia katika kitenzi ‘*ninaweza*.’ Uambishaji wenye kubainisha mofu rejeshi unapaswa kuzalisha vitenzi ‘*lililoua*’, ‘*kilichokosekana*’ na ‘*ninayeweza*.’

Uambishaji unaochangamanisha aina mbalimbali za vielezi vyta mahali katika sentensi moja umebainika katika matini za MK. Uchangamano huu umeishia kuzua ukakasi wa maana. Tazama mifano ifuatayo:

Baada ya mshtuko wa tetemeko hilo, maelfu walizimia majumbanikwao na wengine wakielekea hospitalini, hotelini na kwenye maduka makubwa...Mjini Palu, Mamia ya watu walikuwa wanajiandaa kwa ajili ya tamasha lililokuwa linatarajiwaa kuanza ijumaa jioni.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*

“Uchaguzi mkuu ujao hautafanyika chini ya katiba ya sasa kwa kuwa tutakuwa na sheria mpya. Kwa nini Ruto anafanya kampeni ya kiti cha urais ambacho hakitakuwepo mwaka wa 2022? Yeye ni kama mwamamumee kipofu aliye kwenye chumba chenye giza akifwata paka mweusi ambaye hayuko **humo**,”

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *tuko.com*

Uambishaji wa kiambishi cha undani wa mahali {—ni} katika nomino ‘majumba’ kunahitaji kwamba kimilikishi -*ao* kiweze kupatanishwa na kiambishi cha undani wa mahali {mu}. Uambishaji wa {ku} ni mkorogo wa mahali kusikodhihirika na mahali ndani katika matini moja. Kulingana na muktadha wa dondoo hili, uambishaji mwafaka unapaswa kuwa ‘majumbani mwao’ badala ya ‘majumbani kwao.’

Hali hii ndiyo inayodhihirika katika matini ya siasaambapo pametumika ‘hayuko **humo**’. Kulingana na matini hii, uambishaji wenyе upatanisho mwafaka unapaswa kuwa ‘hayumo **humo**’. Ni wazi kuwa uambishaji huu mbaya wa viambishi vipatanishi vya ngeli, viambishi virejeshi na viambishi vya vielezi umevuruga mshikamano wa matini na kuishia kutatiza ujumbe.

Matatizo ya Kiuakifishaji

Uakifishaji ni matumizi ya alama za lughaa ili kuibusha maana iliyokusudiwa katika sentensi. Kutokana na majukumu yake mbalimbali, viakifishi huwa na dhima mahsusii ya kuyanikisha ujumbe katika matini. Kwa hiyo, matumizi ya alama za lughaa mahala pasipofaa huvuruga maana na kuathiri ujumbe.

Changamoto ya kiuakifishi imedhihirika kutokana na matumizi mabaya ya herufi ndogo. Alama hii imepewa dhima isiyo yake ya kuendeleza nomino za pekee. Mifano ifuatayo inabainisha hali hii.

Marekani imepiga marufuku uagizaji wa nguo kutoka Rwanda, baada ya taifa hilo la Afrika Mashariki kupigamarufuku uingizaji wa mitumba na viatu nchini humo kutoka **marekani**...Mwaka 2016, majirani wa Afrika mashariki Kenya, Tanzania na Rwanda zilikubaliana kupiga marufuku nguo zilizotumika pamoja na viatu kufikia 2019 ili kulinda viwanda vya nchini.

Chanzo: Matini ya kiuchumi kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Huenda *waziri* wa fedha Henry Rotich na aliyekuwa *waziri* wa *viwanda* Adan Mohamed anayehudumu kama *waziri wajamii* ya Afrika Mashariki wakafutwa kazi ikiwa watapatikana na hatia kwenye sakata ya sukari iliyoifanya serikali kupoteza KSh 10 bilioni za ushuru...Kamati za *kilimo* na *biashara* zinazoongozwa kwa pamoja na wenyekeiti Kanini Kega (mbunge wa Kieni) na Adan Ali (mbunge wa Mandera Kusini) zilifichua

kuwa kampuni 14 zilihusika kuingiza sukari nchini kwa njia haramu...Hapo awali, waziri Mohammed alitofautiana vikali na mwenzake wa **usalama** wa **ndani** Dkt. Fred Matiang'i alipodai kuwa sukari hiyo haikuwa na chembechembe za zebaki.

Chanzo: Matini ya kiuchumi kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Mojawapo ya uamilifu wa herufi kubwa ni kutanguliza nomino za pekee. Nomino hizi zimeendelezwa kimakosa kwa herufi ndogo. Nomino za pekee zilizoendelezwa kwa herufi ndogo mwanzoni katika jedwali hili zinajumuisha majina ya nchi (**marekani**), majina ya miungano ya kikanda (Afrika **mashariki**), majina ya nyadhifa za serikali (**waziri wa jamii** ya Afrika Mashariki, **waziri wa fedha** Henry Rotich, **waziri wa viwanda** Adan Mohamed, **waziri wa usalama** wa **ndani** Dkt. Fred Matiang'i), majina ya kamati za bunge (Kamati za **kilimo** na **biashara**) na majina ya mashindano ya mchezo (**kombe la dunia**). Hatua ya kuendeleza nomino hizi za pekee kwa herufi ndogo imedunisha nomino hizi na kuzifanya kuchukua dhima ya nomino za kawaida. Uakifishaji unaokubalika unahitajika kutumia herufi kubwa mwanzoni mwa nomino za pekee ili kuzalisha 'Marekani', 'Afrika Mashariki', 'Waziri wa Jamii ya Afrika Mashariki', 'Waziri wa Fedha', 'Waziri wa Viwanda', 'Waziri wa Usalama wa Ndani' na 'Kamati za Kilimo na Biashara'.

Kwa mujibu wa uchanganuzi huu, ukiushi huu wa kiuakifishaji ambapo alama za uakifishaji ama hazijatumiwa au zimetumiwa katika nafasi isiyofaa umevuruga usomaji wa matini na kuzifanya kutoonekana za Kiswahili. Matumizi haya mabovu yamevifanya viakifishi husika kupoteza uamilifu wake wa kisarufi na hivyo kusababisha upotofu wa ujumbe katika matini.

Matatizo ya Unyambuaji

Mnyambuliko wa vipashio vya lugha ni njia mojawapo ya kuiwamba na kuipanua lugha kimatumizi. Uzalishaji wa ML kwa njia inayofanikisha mawasiliano timilifu unahitaji kuwa lugha itumiwe katika hali mbalimbali ili kuzalisha sentensi nyingi. Hali hizi zinatokana na uambishaji wa mofu mbalimbali katika mizizi ya maneno. Hata hivyo, upungufu wa maana huweza kutokea pale sheria za unyambuaji zimekiukwa. Mifano ifuatayo inaonesha ukiushi huu:

Ruto amekuwa mkoani Pwani **akipatiana** michango katika sherehe tofauti, jambo lilipelekeea Raila kuuliza ni wapi Ruto hutoa kiwango hicho cha pesa **akipatiana** katika michango ya kila wikendi.

Chanzo: Matini ya kisiaa kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Gavana huyo ambaye kwa wakati mmoja aliwahi kuwa msaidizi wa Raila, alisema kuwa itakuwa vema kwa Raila arudishe mkono kwa Kalonzo ila alisisitiza kuwa nafasi hizo kubwa huwa **hazipatianwa** tu ila zinapiganiwa ndiposa zipatikane. "Tiketi za urais huwa hazipatikani

kutokana na hisia, hakuna kitu *hupatianwabure*. Kalonzo na vinara wengine wa NASA watashindana na Raila vivilyo endapo wanataka tiketi za urais katika uteuzi wa vyama,” Ojaamong *aliongezea*.

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Katika matini hizi za siasa, kitenzi ‘*pata*’ chenye maana ya kuwa na jambo, hali au kitu kimenyambuliwa kama ‘*patiana*’ ili kudokeza dhana ya mtu kutoa kitu kwa mwingine. Dhana inayodokezwa katika matini hii ni kuwa kitu kinatoka kwa mtu kuelekea kwa mwingine (Ruto kwa wananchi na viongozi kwa wananchi). Hali hii ya kitu kuelekea upande mmoja tu haiwezi kuwakilishwa na kiambishi kifuutilizi {-i – an –} chenye maana ya mwendo kuelekea pande zote mbili kwa ajili ya mwingine.

Mbali na kutumiwa visivyo kwa kunyambuliwa katika kauli ya kutendeana, kitenzi hiki kimetumiwa visivyo katika kauli ya kutendewa. Katika matini ‘...alisisitiza kuwa nafasi hizo kubwa huwa hazipatianwa tu ila zinapiganiwa ndiposa zipatikane. ‘Tiketi za urais huwa hazipatikani kutokana na hisia, hakuna kitu *hupatianwa bure*’, mfasiri amejaribu kulazimisha uchangamani wa kauli ya kutendeana na kauli ya kutendewa na hivyo kusababisha utata wa kiufasiri.

Ukiushi huu wa kiunyambulishi uloishia kutatiza maana umesababishwa na uteuzi wa kitenzi kisichowenza kutoa dhana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC. Kinachomaanishwa ni kuwa kitenzi ‘*pata*’ hakiweki wazi dhana ya mahala pa kutoa kile anachokihodhi mtu. Kitenzi kinachotoa dhana ya kutoa kitu kwa mwingine ni ‘*pa*.’ Kitenzi hiki kingetumiwa kuzalisha matini kama ‘Ruto amekuwa mkoani Pwani *akiwapa* michango katika sherehe tofauti....’

Kwa upande mwingine, mfasiri angeteua kitezi ‘*toa*’ ili kuhamisha ujumbe uliokusudiwa kwa ukamilifu. Sentensi kama ‘Ruto amekuwa mkoani Pwani *akitoa* michango katika sherehe tofauti, jambo lilipelekea Raila kuuliza ni wapi Ruto hutoa kiwango hicho cha pesa *akitoakatika* michango ya kila wikendi’ na ‘Gavana huyo ambaye kwa wakati mmoja aliwahi kuwa msaidizi wa Raila, alisema kuwa itakuwa vema kwa Raila kurudisha mkono kwa Kalonzo ila alisisitiza kuwa nafasi hizo kubwa huwa *hazitolewi* tu ila zinapiganiwa ndiposa zipatikane. ‘Tiketi za urais huwa hazipatikani kutokana na hisia, hakuna kitu *kinachotolewa* bure. Itabidi Kalonzo na vinara wengine wa NASA washindane na Raila vivilyo endapo wanataka tiketi ya urais katika uteuzi wa vyama’ zingeleweka kwa uwazi zaidi.

Mnyambuliko mwingine uliokengeusha maana katika matini za MK ni wa kauli ya kutendewa. Tazama mifano ifuatayo ya matini:

Haijulikani wazi iwapo Polisi itawasaka mara moja au iwapo *itawapuuzia* tu na kuwaruhusu waendelee na shughuli hizo...Kiongozi huyo wa chama tawala cha ki Liberaliameeleza kwamba sheria za jadi za nchi hiyo dhidi ya matumizi ya bangi hazifanyi kazi, kuzingatia kwamba

raia nchini humo ni mionganoni mwa **wanaotumiwa** kwa kiasi kikubwa bangi duniani. Ameeleza kuwa sheria hiyo mpya imeundwa **kuwaondolewa** watoto bangi karibu, na kuondosha faida wanayoipata wahalifu.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Vitenzi vilivytumiwa visivyo kwenye matini hii ni ‘*tumia*’ na ‘*ondoa*.’ Vitenzi hivi vimenyambuliwa katika kauli ya kutendewa katika matumizi ‘**wanaotumiwa**’ na ‘**kuwaondolewa**.’ Matumizi haya yanapotosha maana ya matini kwa sababu yanadokeza dhana ya ‘kutenda kwa manufaa ya.’ Mnyambuliko wa kauli ya kutenda isiyodokeza athari yoyote kutokana na matumizi ya kimsingi ya kitenzi ungetumiwa katika kitenzi ‘*tumia*’ huku kauli ya kutendea inayotoa dhana ya ‘kutenda kwa niaba ya’ ikiwa sahihi kutumiwa katika kitenzi ‘*ondoa*.’ Kifungu ‘...Kiongozi huyo wa chama tawala cha ki Liberali ameeleza kwamba sheria za jadi za nchi hiyo dhidi ya matumizi ya bangi hazifanyi kazi, kuzingatia kwamba raia nchini humo ni mionganoni mwa **wanaotumia** kwa kiasi kikubwa bangi duniani. Ameeleza kuwa sheria hiyo mpya imeundwa **kuwaondolea** watoto bangi karibu, na kuondosha faida wanayoipata wahalifu...’ kingedumisha maana kwa utoshelevu.

Kadhalika, unyambuaji wa vitenzi ‘*ongeza*’ na ‘*puuza*’ katika kauli ya kutendea katika matini ‘Kalonzo na vinara wengine wa NASA watashindana na Raila vilivyo endapo wanataka tiketi za urais katika uteuzi wa vyama,’ Ojaamong *aliongezea* na ‘Haijulikani wazi iwapo Polisi itawasaka mara moja au iwapo *itawapuuzia* tu na kuwaruhusu waendelee na shughuli hizo’ unapotosha ujumbe. Dhima ya kimsingi ya kauli ya kutendea ambayo ni ‘kutenda kwa niaba ya au badala ya’ haikudhamiriwa katika matumizi haya. Vitenzi hivi vilihitajika kutumiwa katika kauli ya kutenda, yaani ‘*aliongeza*’ na ‘*itawapuuzia*’ ili kuhifadhi ujumbe uliokusudiwa.

Akijadili ukiushi katika matumizi ya kauli ya kutendea, Chacha (2014) anasema kuwa japo sarufi elekezi hutoa kanuni za matumizi sahihi ya lugha, kanuni hizi wakati mwingine hukiukwa na kupuuziliwa mbali kutokana na mitindo kiushi inayosababishwa na sarufi elezi na mabadiliko ya lugha. Hali hii hupelekea utosarufi kukubalika na kuzoleka katika matumizi ya lugha.

Mbali na dhima hii ya kimsingi, kauli ya kutendea huwa na dhima nyinginezko kama vile kufafanua mahali ambapo kitendo kinatokea. Dhima hii imevurugwa katika harakati za kuzalisha ML. Tazama matini ifuatayo ya kiuchumi kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Afrika Kusini, baadhi ya wanafamilia ya Gupta wamekimbia nchini Dubai.

Matumizi ya ‘wamekimbia nchini Dubai’ yanaleta upotofu wa maana ya matini hii. Kiambishi cha kauli ya kutendea {-i-} kimetumiwa katika kitenzi

hiki kama kielezi cha mahali. Hii ndiyo dhana inayowakilishwa na kiambishi tamati {-ni} katika neno ‘nchini.’ Matumizi faafu yanapaswa kuwa ‘wamekimbilia Dubai.’

Kwa upande mwingine, kiambishi {ki} huweza kutumiwa katika mnyambuliko wa nomino ili kuunda vielezi nya namna mfanano kama ilivyo katika ki^{ume}, kitoto na kijeshi. Kwa hiyo, si sahihi kuambisha kiambishi hiki katika vivumishi nya pekee kama njia ya kuunda kielezi cha jinsi. Mfano ufuatao wa matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com* unabainisha hali hii. Obado alielea kuwa hakuhusika **kivyovyote** katika kifo cha Sharon Otieno.

Matini hii inabainisha matumizi ya kiyumishi cha pekee -*o-ote* ili kupata kielezi ‘kivyovyote.’ Vivumishi nya pekee huwa havitumiwi kuunda vielezi nya namna mfanano. Mnyambuliko huu mbovu umevuruga matini na umechangia upotofu wa maana hasa kwa HL inayolelewa LL kwa upana. Matini ‘Obado alielea kuwa hakuhusika **kwa njia yoyote ile** katika kifo cha Sharon Otieno’ ingefaa zaidi katika kuwasilisha maana iliyokusudiwa.

Matatizo ya Hijai

Hijai ni uwakilishaji wa sauti kwa herufi katika maandishi kufuatana na muendelezo wa maneno uliokubalika (TUKI, 2013). Maneno huibua dhana zilizokusudiwa pale yanapoendelezwa ifaavyo. Kwa upande mwingine, upungufu wa kihijai huishia kubadilisha maumbo ya maneno na hivyo kuvuruga maana. Matatizo ya hijai yamedhihirika kutokana na kuendeleza maneno kwa kuyaunganisha visivyo ili kuunda neno moja badala ya maneno mawili, kudondosha baadhi ya sauti na silabi zinazojenga maneno na uchopekaji wa sauti au silabi uliobadilisha maumbo ya maneno. Matini zifuatazo zinadhahirisha ukiushi huu wa kihijai:

Maswali mengi yanazidi kuibuka kutoka kwa walipa ushuru kuhusu manufaa **yamradiwa** reli ya kisasa wa SGR kwa uchumi, wakitaka kufahamu gharama ya mradi huo na kulinganisha na mapato yake tangu Mei 2017.

Chanzo: Matini ya kiuchumi kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Wiki iliyopita Nene aliiambia tume ya uchunguzi wa sakata la akina Gupta ijulikanayo kama tume ya Zondo kuwa aliwahi kuhudhuria kikao na **wafanyabiasharaho...**

Chanzo: Matini ya kiuchumi kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Hatahivyo msemaji wa chama amesema kuwa hajui kile bwana Tendei Biti anachozungumzia...Douglas Mwonzora, afisa wa juu wa chama cha MDC **hatahivyo** aliambia BBC kwamba uungwaji mkono wa mgombea wao na kiongozi wa zamani Robert Mugabe ulikinyima kura chama hicho.

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *bbc.com*.

“Kuna mengi ya **wewekula**. Kuna jumba kuu zaidi ambalo unaweza kumiliki. Kuna ziara nyingi zaidi za kuvutia unazoweza kwenda. Kwa kweli inatosha,” alisema Obama.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Maneno yaliyoendelezwa vibaya kwa kuunganishwa ni kama vile ‘*yamradi*’ badala ya ‘*ya mradi*’, ‘*wafanyabiasharaho*’ badala ya ‘*wafanyabiashara hao*’, ‘*hatahivyo*’ badala ya ‘*hata hivyo*’, na ‘*wewekula*’ badala ya ‘*wewe kula*.’ Maumbo haya yasiyokuwa sahihi yanatatiza usomaji wa matini hizi na kuathiri maana iliyokusudiwa.

Upungufu mwininge wa hijai uliodhahirika ni wa kudondosha baadhi ya sauti na silabi zinazojenga maneno. Udondoshaji huu umeyabadilisha maumbo ya maneno hayo na kuyafanya kuonekana ya ajabuajabu kama inavyojitokeza katika matini zifuatazo:

Taarifa zisizo rasmi kuhusu nia yake ya kujiuzulu zilianza kusikika siku ya jumatatu...**Alikukuliwa** kukubali alikuwa anawapotosha watu licha ya kutokuwepo kwa **ushaidi** wowote wa makosa yake wakati alipokutana na Gupta.

Chanzo: Matini ya kiuchumi kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Aliandana na mkewe pamoja na wanawe wawili akitoa hotuba hiyo...

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Meghan Markle, mkewe Mwanamfalme wa Harry nchini Uingereza ni mja mzito na anatarajiwu kujifungua mwaka ujao wa machipuko, **ksri** la Kensington limefichuwa.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Ishara ni kwamba Raila atagombea tena urais 2022. Tunataka kumweleza mapema kama sasa **asituhebu** kumuunga mkono. Tumempa uungwaji mkono wa kutosha na wakati umewadia tumuunge mkono Ruto,” alisema.

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Everton **hawajawai** kupoteza mechisao tano za kwanza za ligi...

Chanzo: Matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Mifano inayojitokeza katika matini hizi ni ‘*alikukuliwa*’ badala ya ‘*alinukuliwa*’, ‘*ushaidi*’ badala ya ‘*ushahidi*’, ‘*aliandana*’ badala ya ‘*aliandamana*’, ‘*ksri*’ badaya ya ‘*kasri*’, ‘*asituhebu*’ badala ya ‘*asituhesabu*’ na ‘*hawajawai*’ badala ya ‘*hawajawahi*.’ Hijai mbaya iliyodhahirika katika maneno haya imesababisha kupotea kwa maana iliyokusudiwa na mwandishi wa MC.

Kwa upande mwingine, makosa mengine ya hijai yamedhihirika kuitia uchopekaji wa sauti au silabi uliobadilisha maumbo ya maneno. Tazama matini zifuatazo:

Ontario, jimbo lenye idadi kubwa ya watu nchini Canada litaanza **kufunguwa** maduka ya kuuza msimu ujao wa machipuko, licha **ywa** kwamba wateja wataweza kununua bangi kuitia maduka ya mitandaoni.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Kulingana na ripoti hiyo, wawili hao walanza kupokezana mabusu huku mwanamke huyo akizama kwayo na kujisahau. Kwa hali hiyo akawa anamsubiri Kibe ailambe asali. Badala ya kulamba, Kibe aliamua kukiuma kipande cha mzinga na kumuacha mwanamke huyo **akiguguna** kwa machungu na kulowa damu...Polisi **waalimueleza** hakimu kuwa **mshakiwa** huyo mwenye umri wa miaka 40 alifanya kitendo hicho kama njia ya kumuadhibu mwanamke huyo kwa kutokuwa muaminifu.

Chanzo: Matini ya kijamii kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Kutokana na uchopekaji wa sauti za ziada, neno '**kufungua**' limeendelezwa kama '**kufunguwa**', '**ya**' kama '**ywa**', '**akiguna**' kama '**akiguguna**' na '**walimueleza**' kama '**waalimueleza**'. Kadhalika, tatizo jingine la hijai lilihusu ubadilishaji wa sauti katika umbo la neno. Mfano uliodhihirika katika matini hizi ni wa kuendeleza nomino '**mshukiwa**' kama '**mshakiwa**' .

Wakati mwingine maumbo badili ya baadhi ya maneno yanayoendelezwa visivyo husadifiana na maumbo ya maneno mengine ya Kiswahili katika hali zao za kimsingi au katika hali zao za kimatumizi. Hivi ni kusema kuwa makosa ya hijai yamesababisha udhihirishaji wa maumbo ya kimofolojia yaliyopo katika LL. Tazama matini ifuatayo.

Mnao siku ya Jumapili, Julai 8 naibu rais Willian Ruto alikiri kuwa reli hiyo ina gharama kubwa ila akaonyesha matumaini kuwa Wakenya hivi karibuni wataanza kufurahia matunda ya mradi huo.

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *tuko.com*.

Akiwa Gupta pia yadaiwa walikuwa na ushawishi katika uteuzi wa baraza la mawaziri.Ushawishi huo wa kina Gupta ultafsiriwa kama 'kutekwa nyara' kwa serikali ya Zuma...

Chanzo: Matini ya kisiasa kutoka jukwaa la *bbc.com*.

The Blues wa Chelsea tayari wamefikia makubaliano ya kuwasili kwa Sarri mwenye umri wa miaka 59. Iwapo usajili wa Sarri **utadhibitishwa**, atakuwa mkufunzi wa tisa wa Chelsea tangu Mrusi Roman Abramovich aliponunua timu hiyo 2003.

Chanzo: Matini ya michezo kutoka jukwaa la *bbc.com*.

Kwa mujibu wa matini hizi, maumbo badili yaliyosadifiana na maumbo ya maneno mengine ya Kiswahili yameendeleza maneno ‘*mnao*’ badala ya ‘*mnamo*’, ‘*akiwa*’ badala ya ‘*akina*’, ‘*utadhibitishwa*’ badala ya ‘*utathibitishwa*’ na ‘*akiguguna*’ badala ya ‘*akiguna*.’ Mshabaha huu wa maneno uliosababishwa na maendelezo mabaya yameishia kukanganya na kutatiza maana hata zaidi.

Baadhi ya changamoto za kisarufi kama vile makosa ya kiupatanishi, kiuakifishaji, kihijai na mnyambuliko inawezekana yamesababishwa na muda mchache alio nao mfasiri kuhariri kazi yake. Kwa sababu HL aghalabu hutarajia taarifa hai, wafasiri hutafsiri na kuzirusha mtandaoni punde tu zinapochipuka. Kwa upande mwingine, inadhihirika kuwa baadhi ya wafasiri hawana umilisi mpana wa kanuni za sarufi za LL. Ili kuchakata tafsiri wasilifu, nadharia ya Ufasiri hushikilia kuwa mfasiri anahitajika kuwa na umilisi mpana wa LL na uwezo wa kutumia kanuni za sarufi za lugha hiyo ili kuzalisha matini zenye mshikamano.

Hitimisho

Matini hii imeangazia jinsi ukiushi wa kisarufi katika tafsiri unavyoathiri maana ya ML. Ukiushi uliotatiza maana ya matini zilizotafsiriwa katika MK ultokana na tofauti za kiisimu kati ya LC na LL zilizopelekea miundo na ruwaza za kisintaksia za LC kulazimishwa katika LL, makosa ya kiupatanishi, kiuakifishaji, kiunyambulishi na ya kitahajia. Imebanika kuwa mchakato wa tafsiri haufaulu tu kutokana na uteuzi wa vipashio mwafaka na amilifu katika LL bali pia kuhitaji uzingativu wa kanuni za sarufi za LL katika uzalishaji wa ML. Kwa vile tafsiri ni muhimu sana katika kuhamisha habari, maarifa na ujuzi kutoka lugha moja hadi nyingine, makala haya yanapendekeza kwamba wataalam na wanahabari wanaofanya tafsiri katika MK wamakinike zaidi ili waepuke kupotosha ujumbe unaohawilishwa kutoka LC hadi LL.

Marejeleo

- Cartford, J. (1965). *Linguistic Theory of Translation*. London: Oxford University Press.
- Chacha, L. M. (2014). ‘Najivunia kuwa Mkenya: Utosarufi, Mtindo au Mabadiliko ya Lugha?’ Katika Simala, I., Chacha, L. na Osore, M. (Wah.). *Miaka Hamsini ya Kiswahili Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. Kur. 179-187.
- Halliday, M. A. K., McIntosh, A. & Strevens, P. (1964). *The Linguistic Science and Language Teaching*. London: Longman.
- Kihore, M. (2005). ‘Uzingatifu wa Sarufi katika Tafsiri.’ *Swahili Forum 12*, pp. 109-120.
- Larson, M. L. (1984). *Meaning Based Translation: A Guide to Cross-Language Equivalence*. New York: University Press of America.
- Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. Dar es Salaam: TUKI.

- Mwansoko, H. J. M. (2016). ‘Ukuzaji wa Kiswahili kupitia Tafsiri: Hatua Moja Mbele, Mbili Nyuma’. Katika Jilala, H. (Mh.) *Nadharia za Tafsiri, Ukalimani na Uundai wa Istihahi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company Limited. Kur 2-18.
- Myachina, E. N. (1981). *The Swahili Language*. Thetford Norfolk: Thetford Ltd.
- Newmark, P. (1988). *Aproaches to Translation*. London: Prentice Hall.
- Nida, E. A., & Taber, C. R. (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E. J. Brill.
- Oduori, W. R. (2008). ‘Uchunguzi wa Nadharia za Tafsiri: Mwelekeo wa Kiusemezano.’ Katika Ogechi, N. O., Shitemi, N. L. na Simala, K. I. (Wah.). *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika*. Eldoret: Moi University Press. Kur. 333-341.
- Safko, L., & Brake, D. (2009). *The Social Media Bible. Tactics, Tools and Strategies for Business Success*. New Jersey: John Wiley and Sons.
- Seleskovitch, D. (1968). *Language, Langue et Memoire*. Paris: Minard Letters Modernes.
- Shitemi, N. L. (2007). ‘Taswira za Tafsiri, Mielekeo ya Ufundishaji na Maendeleo katika Taaluma ya Kiswahili’. Katika Njogu, K. (Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications. Kur 135-157.
- Tam, J. W., Tang, W. S., & Fernando, D. J. S. (2007). The Internet and Suicide: A Double Edged Tool. In *European Journal of Internal Medicine*, 18: 453-455. New York: Oxford University Press.
- TUKI (2013). *Kamus ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Tatu. Dar-es-Salaam: Oxford University Press, East Africa Ltd.
- Wanjala, F. S. (2011). *Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa Shule, Vyuo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers.
- Waters, J. K., & Lester, J. (2010). *The Everything Guide to Social Media: All You Need to Know about Participating in Today's Most Popular Online Communities*. Avon, MA: Adam Media.
- Wills, W. (1983). *Decision Making in Translation*. In Mona, B. (Ed.). London: Routledge.